Wakulima Wa Mara
Cooperative Union Limited
WAMACU LTD
S.LP 228 TARIME, E-mail. info@wamacu.co.tz TIN 138950433

**MUHUTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI YA WAMACU LTD KILICHOFANYIKA TAREHE 05/07/2023 KWATIKA OFISI ZA WAMACU LTD**

**“MAHUDHURIO”**

| | JINA | | WADHIFA |
|---|---|---|---|
| 1. | Samwel Gisiboye Marwa | - | Mwenyekiti |
| 2. | Bashiru Namchambe | - | Katibu |
| 3. | Mohamedi Sakilu | - | Mjumbe |
| 4. | Brighton Kaimukilwa | - | Mjumbe |
| 5. | Peter C. Wambura | - | Mjumbe |
| 6. | Simion Charles | - | Mjumbe |
| 7. | Joseph Fanuel | - | Mjumbe |
| 8. | Daniel Chacha | - | Mjumbe |
| 9. | Elius Samwel Marwa | - | Mjumbe Wa Bodi Wamacu |

**WAJUMBE WENGINEO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | John Kisege | - | Muwakilishi Idara ya Ulinzi |
| 2. | Aristar Kamanzi | - | Muwakilishi Kutoka Ace Global |

**AGENDA ZA KIKAO.**

1. Kufungua kikao
2. Kujadili shughuli za maendeleo ya ofisi
3. Kupokea wageni kutoka mamlaka ya udhibiti ubora wa mbolea Tanzania(TFRA) kanda ya ziwa na mgeni kutokea kampuni ya Veridoc
4. Kufunga kikao.

**AG.Na.01: KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu wa kikao alisimama na kuwasalimia wajumbe wa kikao kwa salamu ya ushirika na baada ya salamu aliwafahamisha wajumbe kuwa ni kikao cha Menejimenti kwa ajili kujadili shughuli mbalimbali za kiutendaji zinazofanywa na Chama, Na baada ya hayo alimkalibisha Mwenyekiti wa kikao **Ndg. Samwel Gisiboye Marwa** Kufungua kikao

M/kiti **Ndg. Samwel Gisiboye Marwa** alisimama na kufungua kikao mnamo saa tatu kamili (09:00) asubuhi kwa kuwasalimia wajumbe wa kikao na kabla ya kuanza kwa AGENDA za kikao M/kit alitoa taarifa fupi juu ya Salamu za rambirambi na kupongeza wajumbe juu ya ushirikiano uliotolewa kuanzia kwa **Ndg. Olais Piniel, George Kihiri** na **Mariba Mkunyi Baru** walioondokewa na wapendwa wao na Taarifa juu ya kifo cha aliye kuwa katibu wa Nyakonga Amcos **Ndg Daudi Chacha.** Pia aliruhusu Ndugu wajumbe wote kujitambulisha kwa ufupi ili kuweza kufahamiana.

**AG.Na.02. KUJADILI SHUGHULI ZA MAENDELEO YA OFISI**

Katibu alisoma Agenda hii na baadae na kuruhusu M/kiti kuendelea na mjadala, ambapo M/kiti aliwaeleza wajumbe wapya wa kikao juu ya miongozo ya utumishi wa Chama ambapo alitaka wajumbe kufahamu haki zao za msingi kama mtumishi wa chama na kuwataka kutambua na kuzingatia vitu vya msingi wakati wa kutoa huduma za chama kwa wakulima. Pia M/kit aliendelea kwa kusisitiza uaminifu na kujiamini katika utendaji wa kazi, kujali na kuhudumia wateja kwa utaratibu ulio mzuri bila kuwafokea.

Aidha M/kiti aliwataka ndugu Wajumbe kutoka idara ya kilimo kufahama juu ya takwimu za Mahitaji ya mbegu katika kila chama cha msingi AMCOS ili ziweze kusaidia katika kufanya maagizo (order) ya pembejeo hizo kutoka kwa msambazaji (Supplier) na Miche iliyokopeshwa na Chama kwa wakulima wake na kujua mbinu gani mahususi itatumika kwa ajili ya kurudisha fedha ya Chama ambayo ilikua fedha ya mkopo kutoka Benki ya Kilimo TADB.

Pia M/kiti aliwaagiza ndugu wajumbe kuongeza ufanisi katika zoezi zima la uuzaji wa Mbolea ya ruzuku aidha aliwataka watoa huduma ya Mbolea kuhakikisha wanafuata taratibu zote zinazotolewa na mamlaka ya udhibiti ubora wa mbolea Tanzania (TFRA). Hata hivyo mjumbe **Ndg. Daniel Chacha** alichangia juu ya usalama wa fedha za mbolea na kuomba kuwa fedha ziwe zinawekwa kwa awamu tofauti tofauti (installments) ili kupunguza kiwango cha uhatarishi (Risk) cha fedha na Mtunzaji wa fedha hizo. Aidha aliitaka idara Ukaguzi kuhakikisha inafanya ukaguzi kahawa, fedha zilizopo kwenye kasiki na kufahamu kasiki zinazofanya kazi na zisizofanya kazi katika vyama wanachama. Na alimkumbusha mjumbe **Ndg. Alistar Kamanzi** (Ace Global) juu ya suala zima la mtiririko na utoaji wa taarifa na kumtaka kushirikiana na wajumbe wengine wakati wa utoaji taarifa ili kuhakikisha tunafanyakazi kwa ufasaha kama timu moja.

**MAAZIMIO**

1. Wajumbe kwa pamoja waliazimia takwimu za Miche zipatikane na kutafuta mbinu ya kuhakikisha Fedha za chama zinakatwa kutoka wa wakulima walio kopeshwa miche.
2. Zitafutwe Takwimu juu ya kiwango cha Mahitaji ya mbegu na aina ya mbegu inayohitajika kutoka Amcos vyama wanachama.

3. Fedha zote za mbolea zilizokusanywa ziwekwe katika Akaunti ya **WAMACU PEMBEJEO** aidha ikitokea kuna mahitaji ya kuzitumia Mhasibu anatakiwa kuziomba na kuhakikisha anazirudisha katika Akaunti ya pembejeo siku inayofuata tu baada ya kufanya Matumizi.
4. Katika kuhakikisha Mteja anapata huduma bora wajumbe waliazimia Kutengeneza eneo/ kutenga eneo la kivuli na Benchi kwaajili ya wakulima kupumzika wakisubiri kuhudumiwa pembejeo.
5. Ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wajumbe kwa pamoja waliazimia vyumba vya ofisi vifanyiwe marekebisho na meza mbili na viti vinunuliwe kwaajili kuongeza vyumba vya ofisi kwa watumishi.
6. Wajumbe kwa pamoja waliazimia idara ya Ukaguzi kufuatilia Kasiki za vyama wanachama na kubaini ni ngapi zinafanya kazi na ngapi zinahitaji marekebisho.

**AG.Na.03. KUPOKEA WAGENI KUTOKA MAMLAKA YA UDHIBITI UBORA WA MBOLEA TANZANIA KANDA YA ZIWA NA MGENI KUTOKEA KAMPUNI YA VERIDOC**

Katibu alisoma Agenda hii na baadaye na kuruhusu M/kiti kuendelea na Agenda hii, ambapo M/kiti alitoa taarifa juu ya ujio wa Wageni kutoka TFRA kanda ya ziwa ambao walikuja rasmi kwa aajili ya utoaji wa mafunzo kwa watoa huduma ya ugawaji wa mbolea ya ruzuku hivyo basi na kuwataka wajumbe kuwa tayari kwa elimu na mafunzo yatakayotolewa na wageni hao.

Pia alitoa taarifa kwa ujio mtaalam wa kutoka taasisi ya Veridoc **Ndg. Msajigwa A. Kasambo** aliekuja kwaajili ya kutoa elimu ya matumizi ya tovuti ya Wamacu ltd na Matumizi ya mfumo wa **e- finance**

**MAAZIMIO**

Wajumbe kwa pamoja waliazimia kuwa tayari kupokea elimu na mafunzo kutaka kwa wageni wa

**AG.Na.04. KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti **Ndg. Samweli Gisiboye Marwa** alisima na kuwashukuru Wajumbe wa kikao kwa kukubali kujadili AGENDA hii muhimu ya kikao menejimenti na kutoa michango ya muhimu katika kujadili shughuli za maendeleo maendeleo mbali mbali ya Chama. Baada ya kusema hayo aliahirisha kikao mnamo saa tano kamili (11:00) asubuhi na kuwatakiwa wajumbe kazi njema katika Majukumu yao.

***Muhtasari huu umesainiwa kwa niaba ya wajumbe na:***

| | |
|---|---|
| ............................................... | ....................................... |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

LEO TAREHE………….…………….